

Kifaa kisichostahili

Kila wakati kumbuka

- Kudhibiti kiwango kizuri cha maziwa huanzia shambani.
- Maziwa safi ni muhimu kwa kiwango safi na usalama
- Kuyaweka maziwa kwenye barafu ni muhimu na salama.
- Kuyaweka maziwa barafuni huzuia uharibifu.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Omondi S.P.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Muguga North

S.L.P. 32 Kikuyu 00902

Simu: 066 32106/7,32000


Nukulishi: 066 32450

Baruapepe: vrckari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 34 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Jinsi ya kuzuia uharibifu wa maziwa yaliyokamuliwa



Uharibifu wa maziwa ni nini?

Huku ni kuchanganyika kwa maziwa na vitu vingine au virusi vinavyosababisha magonjwa kwa watumiaji. Kuchanganyika na uharibifu huu hutokea kabla ya kukamuliwa hadi wakati wa kuyatumia.

Maziwa yaliyochanganyika na kuharibika hukataliwa na wenye viwanda, mashirika ya maziwa na hata wateja na kusababisha hasara kwa mkulima.

Maziwa yaliyoharibika yana dalili nyingi zikiwemo:

- Chembechembe au kuwa rangi ya manjano hadi hudhurungi
- Chembe chembe yanapochemshwa
- Harufu mabaya
- Huonekana majimaji.

Sababu za uharibifu wa maziwa

Kuna sababu kadhaa zinazoweza kusababisha uharibifu. Baadhi ya hizo ni:

Ng'ombe mwenyewe

Ng'ombe aweza kukusanya matope, au kinyesi kutoka kwa zizi lililojengwa vibaya ambayo yanaweza kuharibu maziwa.

Magonjwa ya ng'ombe kama vile ugonjwa wa matiti pamoja na masalia ya dawa yaweza kusababisha uharibifu wa maziwa.

Mwenye kukamua

Iwapo kiwango tosha cha usafi hakikudumishwa na mkamua uharibifu waweza kutokea. Kiwango kibaya cha usafi ni kama vile kutonawa mikono kabla ya kukamua pamoja na kutumia vyombo chafu au visivyofaa, miongoni mwa sababu zingine.

Mazingira

Virusi vya magonjwa, ladha ya vyakula pamoja na kinyesi au mchanga kutoka kwa kibanda cha ng'ombe yaweza kuharibu maziwa.


Hatua ya kuzuia au kupunguza uharibifu zinaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

Sababu mianza na uzuizi

Sababu	Chanzo cha uharibifu	Namna ya kuzuia
Ng'ombe	Mchanga, vumbi, matope, kinyesi	- Osha matope kutoka kwa ng'ombe. - Osha matiti ukitumia kitamba kilichotumbukizwa ndani ya maji moto.
	Magonjwa k.m. Ugonjwa wa matiti	- Nyoa nywele kwenye matiti. - Hifadhi usafi. - Watibu ng'ombe. - Wachinje ng'ombe wasiopona ili kuzuia uambukizaji.
	Masalia ya dawa katika kuwatibu wanyama	Zingatia kipindi ambacho dawa instahili kuwa imekwisha mwilini.
Mkamuaaji	Kiwango duni cha usafi	- Osha mikono kabla ya kukamua. Hakikisha kucha zimekatwa. - Kata kucha ziwe fupi. - usikamue iwapo wewe ni mgonjwa. - Isichemue, kukohoa, kutemamate wala kuvuta sigara kwenye maziwa.
Vifaa vya maziwa	Vifaa visivyofaa na usafi	- Osha vifaa vya kukamua ukitumia maji safi tena moto.
Bakteria, vigandishi pamoja na kuvu	Kumweka ng'ombe katika chumba kichafu	- Ezeka vizuri na kuwe na sakafu ya sementi katika chumba cha ng'ombe. - Vyombo safi vya chuma vya kuhifadhi maziwa. - Yahifadhi maziwa katika jokofu, maji katika bilauri kubwa au kwenye barafu ya makaa yaliyoloweshwa.
Uchafu	Mchanga Kinyesi	Dumisha kibanda safi cha ng'ombe.
Kutoka kwa ladha	Chakula chenye harufu, kutosafisha vyombo vizuri au/ pamoja na dawa za wadudu	- Epuka chakula cha mifugo chenye harufu kali au malisho yaliyokuwa yamefunikwa masaa mawili kabla ya kuwakamua. - Usiyahifadhi maziwa karibu na mahali penye rangi isiyokauka.

Hatua za kupunguza uharibifu

- Tumia maji yaliyochemshwa, kila wakati kunawa mikono na matiti kabla ya kukamua.
- Tumia kitambaa safi kuosha na kukausha matiti ya ng'ombe.
- Kamua tone la kwanza kutoka kila titi kwenye buti nyeusi ili kuchunguza chembe au rangi nyekundu hadi hudhurungi ambavyo ni dalili za ugonjwa wa matiti.
- Chunga maziwa kwa kutumia kitamba chepesi au kichungi.



Kifaa kinachostahili

- Funika maziwa na uyapeleke mahali safi na baridi.
- Ng'ombe mwenye ugonjwa wa matiti akamuliwe mwisho kasha matiti hayo yatibiwe na maziwa hayo kutupiliwa mbali.

Kupima uzuri wa maziwa

Ukishuku kuwa ng'ombe wako ana ugonjwa wa matiti bila kuziona dalili:

- Chukua sampuli ya maziwa kutoka kwa titi unalo dhania na utume kwa mhuduma wa wanyama u mahabara ya utafiti ilio karibu nawe.